# UFUNDISHAJI WA SARUFI KATIKA SHULE ZA SEKONDARI

*F. L. Mbunda**

Somo la sarufi siyo geni katika shule. Ufundishaji wake umekuwa ukiendeshwa tangu zamani kwa kutumia njia na mawazo mbalimbali ya wataalamu. Sarufi za akina Bloomfield, Ashton, Loogman na Kopoka zimekuwa zikishughulikia utambuzi wa maumbo na utaratibu wake katika tungo. Ndiyo maana tulipata msamiati wa Jina, Tendo, Sifa (Kivumi), Kisifa, Kimalizio, Kiungo, n.k. Kutokana na msamiati huo tulielekezwa kuona pia kazi au maana ya kila umbo. Swali kama "Sifa ni nini?" lilitaka kujua kazi na maana ya hilo umbo liitwalo sifa.

Leo hii ni lazima tujiulize maswali yafuatayo:

(a) Kuna lazima ya kufundisha sarufi? Kama ndiyo, katika vidato gani?

(b) Sarufi tuliyoipokea hadi sasa inatosheleza haja zetu hususan katika kukichambua Kiswahili?

(c) Iwapo haja ya kufundisha sarufi shuleni ipo, tuifundisheje? Tutumie sarufi gani na njia zipi za ufundishaji?

Katika kujibu maswali hayo, pamoja na mengine mengi itakuwa lazima tuone kwanza mkondo uliochukuliwa katika ufundishaji wa sarufi tangu zama hizo. Tangu hapo zamani, somo la sarufi lilionekana la maana sana kwa sababu zifuatazo:

(a) somo hilo linaadilisha akili;

(b) linaongeza ujuzi wa lugha;

(c) linasaidia ujuzi katika kuandika na kusoma;

(d) linasaidia katika kujifunza lugha za kigeni;

(e) linasaidia kutambua utaratibu wa lugha ulivyo.

Sarufi ya Kilatini ndiyo iliyokuwa msingi wa sarufi ya lugha nyingi. Kwanza ilikuwa muhimu sana kujifunza na kujua Kilatini. Halafu nchi fulani zilipoamua kutumia lugha zao katika ufundishaji zilitumia utaratibu wa lugha ya Kilatini. Shule zilizofundisha sarufi mithili hiyo zilikuwa na sifa za pekee, na hata leo kuna nchi ambazo shule kama hizo ziitwazo *'Grammar Schools'* bado zipo.

Sarufi katika misingi ya Kilatini ndiyo tunayoiita sarufi ya mapokeo. Vipengee vya sarufi hiyo ni:

(a) Haina utaalamu wa kisayansi ndani yake. Maelezo yaliyotolewa mara nyingi hayakuhusiana na uchunguzi halisi wa lugha iliyokuwa ikitumiwa, k.m. Kiingereza, Kiswahili n.k.

(b) Njia zake za uchambuzi hazikuwa na msimamo maalumu, na hazikuweza kutosheleza uchambuzi wa lugha nyingine. (Taz. jibu la **Noun** ni nini katika vitabu mbalimbali vya Sarufi ya mapokeo, kama vile, *Sarufi ya Kiswahili* cha Bloomfield).

(c) Mara nyingi sarufi hiyo ilitokana na maoni ya mtu binafsi na haikutokana na hali ya lugha ilivyo. Hivyo basi, sheria au kanuni ziliangulia maelezo ya lugha ilivyo.

Baadaye wataalamu mbalimbali wa Isimu na Lugha kama akina Henry Sweet (1891), Otto Jesperson (1894), H.C. Wyld (1925), Lowth Lindley Murray, Sapir na Bloomfield, walianza kuiangalia sarufi kwa macho mengine. Hao waliona kuwa:

(i) Kanuni za sarufi hazina maana yoyote ila ni katika kutaja au kuzijua sheria tu. Kwani, chochote kitumiwacho katika lugha fulani huwa sarufi safi katika lugha hiyo.

(ii) Sarufi haifundishi jinsi ya kuizungumza lugha kama ilivyodhaniwa hapo zamani, bali inaonyesha tu jinsi watu walivyoimudu lugha hiyo wakati ilipoandikwa.

Mwanzoni mwa karne ya ishirini yalizuka mawazo mengine ya sarufi kutokana na mawazo mapya ya Isimu ambayo yalizuka wakati huo. Wataalamu wa karne hiyo hawakutoa maana ya sarufi tu, bali walijadili kazi ya wanasarufi. Hivyo, sarufi ya mapokeo ilivuliwa kofia yake ya kutoka taarifa za juujuu tu. Bwana Wyld ndiye alianza kufikiria zaidi kueleza lugha ilivyo, badala ya kutoa kanuni tu. Huo ulikuwa mwanzo wa kufikiria MAANA katika sarufi licha ya maumbo tu yatoayo maana hiyo.

Sarufi ilielezwa kuwa ni **uchunguzi wa njia ambazo kwazo lugha hufikia muundo wake**. Msingi ulikuwa kuchunguza lugha inavyotumiwa. Maelezo hayo ya sarufi hayakuongelea sarufi nzuri au mbaya bali yalisisitiza kwamba kila kisemwacho katika lugha ilimradi kina shabaha ya kuwasilisha wazo na kutoa maana inafaa kichunguzwe kilivyo.

Kutokana na msingi huo, Mabwana George Trage, Henry Lee Smith na Kenneth Pike walipendekeza uchambuzi wa lugha ufanywe kutokana na tabaka tatu, yaani:

(a) sauti za lugha hiyo;
(b) maumbo yaletayo maana;
(c) tungo (muundo wake).

Hao waliitazama lugha kutokana na muundo wake. Bwana C. Fries (1954) alipendekeza mbinu nyingine za kuutazama muundo wa lugha. Kwake sarufi ni **uchunguzi wa maumbo ya lugha yaashiriayo maana katika muundo wake**. Kutokana na njia mbalimbali ambazo binadamu hutumia lugha, alipendekeza njia tano za uchambuzi katika sarufi yake:

(a) mpangilio wa maneno;
(b) vihusishi katika tungo;
(c) mnyambuliko wa maneno;

(d) miendelezi ya maneno;
(e) kiimbo (shadda, lafudhi, matamshi).

Bwana Fries aliona kuwa kutokana na njia hizo tano tunaweza kupata muundo na maana katika lugha yoyote ile.

Huo haukuwa mwisho wa mawazo katika sarufi. Wataalamu wengine kama Zelling Harris na Noam Chomsky nao wakaja na mawazo mengine. Kwao **sarufi ni mkusanyiko wa sheria maalumu ambazo kwazo zinaweza kuzaa idadi ya tungo zisizo na kikomo katika lugha yoyote ile.**

Wataalamu hao wanazigawa tungo katika aina mbili:
(a) tungo-asilia;
(b) tungo-tokeo.

Kazi kubwa katika sarufi yao ni kuchunguza kanuni zote zinazoweza kuzaa tungo-tokeo kutokana na tungo-asilia. Kwa mfano, **Ali amepigwa na Juma** ni tungo-tokeo ya **Juma amempiga Ali**. Kanuni zinazobadili tungo-asilia hiyo ni kama hivi:
(a) **Ali** inachukua nafasi ya **Juma** na ya **Juma** inachukuliwa na ya **Ali**
(b) Ondoa -m- katika **amempiga** na badala yake weka -w- kabla ya –a ya mwisho na kuunda **amepigwa**
(c) Weka **na** kati ya **amepigwa na Juma**.

Kwa njia hizo tunapata: **Ali amepigwa na Juma** kutokana na **Juma amempiga Ali**. Kwa jina jingine, sarufi hii huitwa **Geuza-tungo**.

Mpaka sasa tumeona sarufi za aina tatu:
(a) **Sarufi ya mapokeo -** uchambuzi uligusia zaidi umbo moja moja na nafasi yake katika tungo.
(b) **Sarufi-miundo -** ilisisitiza muundo wa lugha kutokana na sauti zake, maumbo na tungo. Pia sarufi hii inagusia maana kutokana na jinsi maneno yanavyopangwa, yanavyotumiwa katika mazingira mbalimbali na pia kutokana na kiimbo katika lugha yoyote ile.
(c) **Sarufi geuza-tungo-** inashughulikia sheria ambazo tungo huweza kuzaa tungo nyingine.

Sasa labda tunaweza kujibu yale maswali yaliyotolewa hapo awali.
(a) Kuna lazima ya kufundisha sarufi? Kama ndiyo, ni katika vidato gani? Haja ipo. Tunapenda wanafunzi wetu watambue jinsi lugha yao ilivyo, na kwa nini ina matumizi ainaaina katika nyakati mbalimbali na kwa watu mbalimbali. Kuitumia tu lugha bila kujua misingi yake ni mithili ya kufunga safari ndefu bila kujua madhumuni yake na

wapi tunakwenda na sababu ya safari hiyo. Sababu zilizotolewa hapo awali, kwa mfano, kuadilisha akili, kuongeza ujuzi wa lugha, kukuza ujuzi wa kuandika na kusoma, kusaidia kujifunza lugha za kigeni, hazina uhusiano wowote na ujuaji wa sarufi ya lugha fulani. Sarufi ya lugha moja inaonyesha tu uhusiano tofauti na sarufi ya lugha nyingine. Jibu la sehemu ya pili ya swali la kwanza ni kwamba sarufi ifundishwe katika vidato vyote, bora tu kila kidato kipate mafundisho ya kiwango chake.

(b) Sarufi tuliyoipokea hadi sasa inatosheleza haja zetu hususan katika kukichambua Kiswahili? Jibu ni hapana. Ni wazi kuwa lugha lazima ichunguzwe kadiri ilivyo. Kiswahili kama lugha nyingine kinakua na kubadilikabadilika. Sarufi tuliyoipokea mpaka sasa hailingani kamwe na hali na matumizi ya Kiswahili yalivyo hivi sasa. Hiyo sarufi ya mapokeo, kwa mfano, ilikuwa na ngeli iliyoitwa "U-class." "Ngeli hiyo iliitwa ya "U" kwa sababu Nomino (Majina) zake zilianza na "U". Ndio ukosefu wa kuangalia umbo mojamoja. Hii si kweli hata kidogo kwamba maneno yote yaanzayo na "U" yawe katika ngeli moja bila ya kuangalia matumizi yake. Tukitazama kwa juujuu tunaweza kuyapanga maneno ya namna hiyo katika mafungu manne kama ifuatavyo:

(i) **Ua langu limenyauka-Maua yangu yamenyauka:** ("U"/ "ma" ya vitu halisi)

Maneno mengine katika fungu hili ni: Umiko-maumiko, Umivu-maumivu; Ungo-maungo (Kiungo, sehemu ya mwili) Umbo-Maumbo: Mifano hiyo inakubaliana kimatumizi na ile ya: kasha (makasha), sanduku, kabati, kopo, koti, kofi, n.k.

(ii) **Ugonjwa wangu umepungua-Magonjwa yangu yamepungua:** ( "U"/ "ma" ya vitu dhahania)

Mifano mingine: ubaya-mabaya, ubongo-mabongo, uchochoro-machochoro, udevu-madevu, ufumbi-mafumbi uuguzi-mauguzi, ulaika-malaika, ulalo-malalo, ulili-malili, umoja-mamoja, unono-manono, ununuzi-manunuzi, unyasi-manyasi, unyoya-manyoya, uombi-maombi, uonevu-maonevu, uovu-maovu, upaji-mapaji, upana-mapana, upendezi-mapendezi, upendo-mapendo, upenzi-mapenzi, upishi-mapishi, urembo-marembo, usia-mausia, utembezi-matembezi, utumbo-matumbo, uvuno-mavuno, uwele-mawele.

Vile vile yapo maneno mengi yatumikayo katika uwingi tu, k.m. maji, mafuta, majivuno, masimango, mahindi(mhindi), maziwa n.k..

(iii) **Ufa wangu umezibwa-Nyufa zangu zimezibwa**: ("U"/"n" ya vitu halisi)

Mifano katika kundi hili ni mingi, k.m. ukuta-kuta, uma-nyuma, ubao-mbao, ubavu-mbavu, ufagio-fagio, ufunguo-funguo, ugo-nyugo, n.k.

(d) **Utu wake ulimlinda**: ("U" dhahania isiyo na wingi)
Maneno mengine ni kama ujambazi, uvumilivu, unyanyaswaji, uwongo na mengi mengine.

Wanasarufi kadha walijitetea kwa kusema kuwa baadhi ya maneno, k.m. ugonjwa yalikuwa kivuo (exception) cha ngeli ya "u". Kivuo hicho tutakiwekea maneno mangapi?

Mfano wa hapo juu unaonyesha upungufu wa sarufi ya mapokeo. Ni lazima tutafute mbinu ambazo zitatosheleza sarufi ya Kiswahili. Njia iliyo wazi ni ile ya kuichambua lugha kadiri wenyeji wake wanavyoimudu.

(c) Swali la tatu lilitaka kujua iwapo pana lazima ya kufundisha sarufi, tufundishe sarufi gani na kwa njia zipi? Katika kujibu swali hili itatupasa tuangalie yafuatayo:

(i) Tuichague sarufi ile inayoonekana kutoa fununu zaidi katika uchambuzi kutegemeana na Kiswahili kilivyo. Kwa majaribio, sarufi zote tatu zitafaa katika vidato mbalimbali.
(ii) Sarufi ifundishwe kama utaratibu wa lugha ilivyo.
(iii) Somo la sarufi lichukuane na tungo na maana zake.
(iv) Tungo hizo ziwe zile zinazofahamika kwa wanafunzi. Inafaa kuzitumia tungo zile ambazo wao wenyewe wanazitumia au zile wanazozisoma katika maandishi mbalimbali.
(v) Ufundishaji wa sarufi uanze na mifano, kisha mifano hiyo ichambuliwe, na mwisho zitolewe kanuni zake.
(vi) Mkazo utiliwe katika tungo nzima au maneno na uhusika wake wala si kutumia neno moja moja.
(vii) Vitabu vikitumiwa katika kupata mawazo au mifano, itumiwe kwa uangalifu, yaani ufanywe kulingana na kiwango kilichofikiwa, na kufuatana na lugha ilivyo.
(viii) Sarufi ifundishwe kama sehemu ya lugha sawa na mazoezi mengine kama vile ufahamu.

Kwa kifupi, njia zitakazotumiwa ziwe zile zitakazolingana na hali ya lugha ilivyo. Kanuni zitajitokeza zenyewe baada ya kuchambua mifano mingi katika lugha hiyo.

Ni wazi kuwa hatutaweza kuanza na kitu kipya kabisa. Tutatumia mawazo mengi yaliyotolewa na wataalamu waliotangulia. Jambo kubwa litakuwa katika kuhusisha mawazo hayo na Kiswahili kilivyo na kuiweka maana mbele katika kila somo la sarufi.

Ifuatayo ni ratiba ya masomo ya Sarufi kama ilivyotolewa katika muhtasari wa mafundisho ya Kiswahili - Kidato cha Kwanza mpaka kidato cha Nne. Kutokana na ratiba hiyo kumetolewa mwongozo mfupi kuhusu ufundishaji wa vipengele mbalimbali.

**Kidato cha Kwanza**

1. **Muundo wa Tungo Sahili za Kiswahili:**

(a) Mwalimu awaongoze wanafunzi kutambua muundo wa Tungo Sahili. Mwalimu aandike ubaoni mfano wa Tungo Sahili (Simple sentence), k.m. **MAMA ANAPIKA CHAKULA**. Kisha wanafunzi watoe mifano mingine mingi yenye muundo wa aina hiyo (watoto wanakula chakula, Baba amenunua nguo...).

(b) Baadaye mwalimu awaongoze wanafunzi kutambua maana ya Tungo Sahili ni tungo yenye Kiima kimoja na Tendo moja. Mwalimu aonyeshe Kiima ni nini.

(c) Halafu wanafunzi wafanye mazoezi ya kujazia vipashio vinavyojenga Tungo Sahili, k.m. (i)...... analima shamba

(ii) Dada......... kitabu

(iii) Kaka anakunywa........

(d) Mwalimu awaongoze wanafunzi kutambua makundi ya maneno yajengayo Tungo Sahili, k.m. Mama anapika chakula

= N + T + N

Mama hodari anapika chakula kizuri

= N + S + T + N + S

Jana asubuhi dada yangu mkubwa alichemsha chai

= Ch + Ch + N + S + S + T + N

**kwenye jiko la mkaa**

**+ Ch**

Iwapo kuna N mbili, au S na Ch mbili itafaa ionyeshwe. Mathalan, katika tungo ya: **Mama anapika chakula**, muundo wake ni N + T + $N_2$

Makundi ya maneno yatakayochambuliwa katika Kidato hiki kama yafuatayo:

| | |
|---|---|
| Nomino ambayo inaonyeshwa kwa kifupi na | N |
| Sifa ambayo inaonyeshwa kwa kifupi na | S |
| Tendo ambalo linaonyeshwa kwa kifupi na | T |
| Chagizo ambacho kinaonyeshwa kwa kifupi na | CH |
| Kihusishi ambacho kinaonyeshwa kwa kifupi na | H |

Makundi hayo yakiwa katika tungo tunayaita **vipashio.** Tungo ifuatayo ina vipashio vyote vitano:

**Kitabu chetu kimeliwa vibaya na mchwa hawa**
$N_1$ + $S_1$ + T + Ch + K + $N_2$ + $S_2$

(e) Mazoezi zaidi yafanywe ili kujenga Tungo sahili kwa kutumia:

(i) Maneno kisha vidokezo au vipashio vyake, k.m. Mwalimu wetu ametugawia kazi nzuri = $N_1 + S_1 + T + N_2 + S$

(ii) Vidokezo kisha tungo ya maneno
k.m. N + S + T + Ch = Mwalimu yule alifika jana.

2. **Kuchambua vipashio vijengavyo Tungo Sahili:**

(a) Nomino: Uchambuzi wa ngeli zake ufanywe kufuatana na uhusika wake katika Tendo, k.m.

(i) Mwalimu anafundisha - Walimu wanafundisha
(ii) Mti umeanguka - Miti imeanguka
(iii) Kisu Kimevunjika - Visu vimevunjika
(iv) Ndizi imeiva - Ndizi zimeiva
(v) Kasha limefunguliwa - Makasha yamefunguliwa (angalia: ua - maua, umbo - maumbo...)
(vi) Uzi umekatika - Nyuzi zimekatika
(vii) Ugonjwa umeingia - Magonjwa yameingia
(viii) Uchoyo wake umemponza (hakuna uwingi), n.k.

**Tanbihi:** Sehemu hii ya Nomino imesahauliwa kuwekwa katika Muhtasari mpya.

(b) Sifa: Zipo Sifa zisizochukua kiambisho. Kama vile: Mtoto *hodari/safi*. Jambo *dhahiri/rahisi*. Zipo pia Sifa zinazochukua kiambisho, k.m. Mtoto mpole, mkubwa. Watoto wengi, warefu.

**Aina za Sifa**:
(i) za kumiliki: -angu, -ako, -etu
(ii) za maelezo: -zuri, -baya, hodari,........
(iii) za kuonyesha huyu: yule, huu, hii, ile, wale,......
(iv) za idadi: moja, -ili, -tatu, -ingi, -ote,.........
(v) za kuuliza: -pi, -ngapi,

(c) Tendo: (i) Kwanza waangalie umbo la Tendo, ambalo ni Viambisho +Shina

Kwa mfano: Nitampata
Ni = kiambisho cha Kiima (mimi)
ta = kiambisho cha wakati ujao
m = kiambisho cha mtendewa (yeye)

pata= shina la tendo

(ii) Wanafunzi waongozwe kutambua kuwa Shina la Tendo limegawanyika katika sehemu kuu mbili: Kiini + Kiambisho au Viambisho vya mwisho. Kwa mfano: SHIBA - **Shib** ni Kiini, na **a** ni Kiambisho cha hali timilifu ambayo ni yakinisho. Viambisho vingine ni kama vile **-wa** katika pigwa, **-ilia** katika **pigilia**, **-ainisha** katika **unganisha**, **-ana** katika **fungana**.

(iii) Kutambulisha aina za Tendo. Kuna tendo kuu (T) na tendo saidizi (t). Kwa mfano: **Alikuwa anacheza mpira**, tendo kuu ni **anacheza,** na tendo saidizi ni **Alikuwa**. Muundo wa tungo hii basi ni t + T + N. Tendo kuu ni tendo muhimu katika tungo. Angalia mifano ya tendo saidizi katika muhtasari.

(iv) Uhusika na Tendo: Tendo laweza kumalizika peke yake bila kuchukua Nomino, kwa mfano katika **Juma ameondoka**. Tendo laweza kuchukua Nomino moja, mf: **Juma anakunywa maji** = Tendo + $N_1$. Tendo laweza pia kuchukua Nomino mbili, mf: **Juma amempa mwalimu kitabu chake** = Tendo + $N_1$ + $N_2$.
Mazoezi mengi yafanywe ili wanafunzi waweze kuyachambua matendo katika vipengele hivyo vyote.

(d) Chagizo: Kipashio hiki kichambuliwe kutegemeana na aina zake:
(i) cha wakati - jana, leo, asubuhi...............................
(ii) cha maelezo - haraka, polepole, vizuri, upesi,................
(iii) au cha jinsi
(iv) cha mahali - mezani, kwenye jiko la mkaa, hapa, Tanga..........

(e) Kihusishi: Kipashio hiki hakipo katika ratiba ya Kidato cha Kwanza kwa sababu mara nyingi hakitumiwi katika Tungo sahili. Hata hivyo itafaa kukigusia kidogo hapa iwapo kitatokea katika mifano ya Tungo sahili. Kwa mfano: (i) na: Ameumwa **na** mbwa. Amefuatana **na** babu
(ii) ya, cha, vya, .......Juma amebeba mzigo **wa** kuni. Jengo hili ni mali **ya** umma.

**Tanbihi**: Wanafunzi wapewe mazoezi mengi, na mifano yake itokane na wao wenyewe, au itokane na vitabu makala wasomayo. Mfano wa zoezi waweza kuwa hivi: Kutokana na kifungu ulichokisoma, chagua maneno yote ambayo ni (a) Nomino, (b) Sifa, (c) Tendo, (d) Chagizo, kisha panga kila kundi katika aina zake. Mfano wa majibu:

(a) mazoezi = Nomino, aina ya LI katika umoja, na YA- katika wingi

Ufito = Nomino, aina ya U katika umoja, na ZI-

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | katika wingi |
| (b) | kamili | = | Sifa ya maelezo |
| | huyu | = | Sifa ya kuonyesha |
| (c) | amekwisha | = | Tendo saidizi |
| | atasoma | = | Tendo kuu |
| (d) | polepole | = | Chagizo cha jinsi |
| | ukutani | = | Chagizo cha mahali |

**Kidato cha Pili**

Mwalimu afanye marudio ya muundo wa tungo sahili, hali kadhalika marudio ya vipashio na kazi zake katika tungo.

**Kazi yenyewe:**

(a) Aina ya Tungo za Kiswahili:-
(i) Tungo huweza kuwa HURU. Tungo huru ni ile inayoweza kusimama peke yake, k.m. **Mama anapika chakula**. Tungo yaweza pia kuwa TEGEMEZI. Tungo ya aina hii haiwezi kusimama peke yake, k.m. **Atakapofika, mtoto anayesoma** .....
(ii) Tungo ambatano: ni tungo huru mbili au zaidi, k.m.
**Nilimwita na alifika**.
**Mwalimu aliingia darasani, wanafunzi wote tulisimama na tukamwamkia.**
**Baba na mama wanalima** (m.y. Baba analima na mama analima).
(iii) Tungo mchangamano: ni ile yenye tungo huru na tungo tegemezi pamoja, k.m. **Atakayefanya kazi kwa bidii atapewa tuzo zaidi**.

(b) Wakati wa kuchambua tungo mchangamano mwalimu awaongoze wanafunzi kutambua vitegemezi vifanyavyo tungo iwe tegemezi. Mfano wa vitegemizi ni: *-po, -vyo-, -ye-, ambaye, ijapokuwa, kwa kuwa, kwa sababu, kama*, n.k. (Angalia: *kwa kuwa* na *kwa sababu* vyaweza kuwa vihusisho ambavyo vinaunganisha tungo huru mbili. Mfano huu ni tofauti na: **Hakuja shuleni kwa sababu isiyojulikana**.

(c) Vihusisho vitashughulikiwa zaidi katika Kidato hiki. Vihusisho vinatumiwa zaidi katika tungo ambatano na tungo mchangamano. Kwa mfano wa vihusisho katika tungo sahili taz. 2-e katika Kidato cha Kwanza).

Mazoezi yafanywe kutokana na tungo watakazozisoma vitabuni mwao papo hapo wakikamilisha kazi ya Kidato cha Kwanza. Baada ya mwaka wa pili itategemewa kuwa wanafunzi watakuwa na ujuzi wa kuzichambua tungo na kuzipanga

katika aina zake.

**Kidato cha Tatu**

Kazi kubwa katika Kidato hiki ni kuchambua miundo mbalimbali ya maneno ya Kiswahili, na jinsi yanavyofanya kazi katika tungo ili kuleta maana mbalimbali. Itambidi mwalimu awaongoze wanafunzi kutambua njia mbalimbali ambazo kwazo maneno ya Kiswahili huundwa. Njia hizo ni:

(a) Kwa kutumia mpangilio wa vitamkwa, k.m. pata, nata, kata, bata, hata, mata, n.k.
toa, tao, ota
sita, tisa, tasi.
Ikumbukwe kwamba vitamkwa katika kila mfano havina uhusiano, bali hiyo ni njia ya jumla tu ya kuona jinsi maneno yanavyojengwa hata yakaleta maana tofauti.

(b) Kwa kutumia minyambuliko ya maneno:
Tendo: cheza - mchezo, mchezaji, mchezeshaji;
cheka- mcheshi, mchekeshaji, mcheko, kicheko.
Nomino: haki - stahiki, hakiki, hukumu husudu-husuda.
Sifa: huru - uhuru, huria, huri, peke - pekee, upweke, peka, mpweke.
Chagizo: upesi - upesi, wepesi.

(c) Kwa kutumia miendelezo ya maneno katika:
(i) Tendo - funga, fungia, fungana, fungisha, fungika, fungwa, fungamana.
(ii) Nomino - haki, hakimu, hakika, uhakika, hukumu

(d) Kwa kutumia miambatano ya maneno:
(i) N + N - mwanahewa, afisaelimu, binadamu, mwanasesere
(ii) N tegemizi + N huru - kifunguakinywa, kiinuamgongo;kivunja- jungu, kizamiadagaa, kinasasauti, kionambali, kiangazamacho, kionjamchuzi
(iii) T + N - zimamoto, pimamaji, ndumakuwili
(iv) N + S - fungule, babake, mwanao, nduguze

(e) Kwa kurudiarudia maneno - polepole, mbalimbali, chezacheza, tangatanga, metameta.

(f) Kwa kutumia mchanganyiko wa maneno mbalimbali:
msikwao - mtu asiye na kwao
nyamafu - mnyama aliyekufa (mfu)
mahakama- mahali panapotolewa haki/hukumu?
jamhuri - jamii/jumuiya iliyo huri/huria/huru
maneno kama: mkurugenzi, mkurufunzi, mkufunzi, yaangaliwe
kwa njia hiyohiyo ya mchanganyiko wa maneno.

Kazi ya mwaka huu itasaidia sana katika kupata maana ya maneno

yasomwayo. Ijulikane wazi kuwa lugha haina mipaka. Matumizi yake ni mapana sana. Hivyo wanafunzi waelekezwe kuona vidokezo, mathalan, kiini/viini vya maneno ambavyo vitasaidia kupata maana ya maneno hayo, pia wanafunzi waelewe maana ya viambisho mbalimbali ambavyo vinaambatana na viini vya maneno yatumikayo; mf. **Alipata aibu sana kwa jinsi walivyomdunisha**. Wanafunzi hapa waelewe kuwa **dun** ni kiini cha DUNI, na **isha** ni kiambisho chenye maana ya kufanya kuwa na hali fulani, kama hivi kufanya kuwa duni. Kwa njia hii basi maana zitapatikana kutokana na maneno yalivyotumiwa bila kutegemea sana msaada wa mwalimu, au kutoka katika kamusi.

**Kidato cha Nne**

Katika Kidato hiki wanafunzi watafundishwa vipengele vitatu vya sarufi ya Kiswahili:-

(a) Mchanganuo wa Tungo:
Tunazichanganua tungo na kuona kanuni zake katika kauli ya Kutenda (*amempiga Ali*), ana kauli ya Kutendewa (*amepigwa na Juma*) katika
- (i) maelezo - Amekwenda sokoni
- (ii) maulizo - unakwenda wapi?
- (iii) amri - Njoo hapa
- (iv) ombi - Tafadhali uje hapa

Kisha kila tungo itazamwe na kuonwa kanuni zake katika hali **YAKINISHO** (*amekwenda sokoni*) na hali **KANUSHO** (*hakuenda sokoni*).

**Mfano wa zoezi la Tungo za maelezo:**

Paka atamla panya - kauli ya kutenda, tungo yakinisho
Panya ataliwa na paka - kauli ya kutendewa, tungo yakinisho
Paka hatamla panya - kauli ya kutenda, tungo kanusho
Panya hataliwa na paka - kauli ya kutendewa, tungo kanusho.

Kila mwalimu anaweza kutumia mpango wake, bora tu kila tungo inachambuliwa katika vipengele vyake vyote.

(b) Mpambanuo wa Uhusika katika Tungo:
Tunapambanua tungo kufuatana na uhusika wake wa
- (i) Kiima na Prediketa. Wanafunzi watambue maana ya Kiima na Prediketa kutokana na uwezo wao wa kutenganisha vitu hivi viwili katika mifano mbalimbali, mathalan:

| KIIMA | PREDIKETA |
|---|---|
| Mjamaa<br>Mjamaa halisi<br>Mtoto mvivu<br>Kazi iliyo nzuri<br>Yule ndugu<br>n.k. | Hufanya kazi kwa bidii<br>Hufanya kazi bila kuchungwa<br>Hastahili sifa yoyote<br>huleta mafanikio mazuri<br>atakamatwa sasa hivi |

(ii) Kutokana na mifano hiyo na mingine ya wanafunzi, mwalimu awaongoze kutambua muundo wa Kiima na ule wa Prediketa. Kwa mfano, kutokana na tungo za hapo Kiima chaweza kuwa
- N (Mjamaa)
-N + S (Mjamaa halisi, Mtoto mvivu)
-S + N (Yule ndugu);

Prediketa yaweza kuwa na
- T (amekwenda)
-T + N (huleta maendeleo)
-T + N + S (huleta mafanikio mazuri)
-T + CH (atakamatwa sasa hivi).

Mpambanuo wa uhusika katika tungo waweza kufanywa kwa njia zifuatazo:

| KIIMA | | PREDIKETA | | |
|---|---|---|---|---|
| **Nomino** | **Sifa** | **Tendo** | **Nomino** | **Sifa** |
| Kazi<br>ndugu<br>n.k. | iliyo nzuri<br>yule | Huleta<br>Atakamatwa | Mafanikio | Mazuri |


Au:

**Kiima**

| Kazi | iliyo nzuri |
|---|---|
| N | S |

**Prediketa**

| huleta | maendeleo | mazuri |
|---|---|---|
| T | N | S |




(c) **Dhana ya "KUWA na "KUWA NA".**

Kipengele hiki kina mifano ya kutosha katika muhtasari mpya uliopigwa chapa na PRINTPAK/MTUU, Dsm, 1976, uk. 15-16. ila tu patatakiwa kuwa na marekebisho kwenye dondoo 3.2.1., uk. 16 kama ifuatavyo:

Kiambishi + wakati + KUWA, mfano:
Yakinishi: anaKUWA mkali kila siku
Kanushi: hawi mkali kila siku
(mengine yote ni sawa)

## Marejeo


Chama cha Kiswahili, Chuo Kikuu cha DSM, *Kioo cha Lugha*, Toleo 4-6.

Halliday na Wenzake. The Linguistic Sciences and Language Teaching. London: Longmans

Herndon, J.H. (1970) A survey of *Modern Grammars* NY: Holt, Rinehart & Winston Inc.

Langacker, R.W. (1968) *Language and Its Structures*, Part II NY: Harcourt, Brace and World Inc.

Lyons, J. (1970) Chomsky. Katika M.A.K.

Palmer F. (19884) *Grammar* London penguin Books

Postman N. na Charles Weingarter (1966) *Linguisics:*A revolution in teaching.NY: Delacorte Press

Stervens, P. (19665) Papers in Language and language teaching. London: OUP

Wizara ya Elimu ya Taifa (1976) Languages syllabi (Muhtasari wa Masomo ya Lugha). PRINTPAK/MTUU


* *Makala haya yalitolewa kwa mara ya kwanza katika MULIKA Na.9.*